

DOCUMENT RESUME

ED 402 737

FL 024 285

AUTHOR Simba, Esther M.; And Others
TITLE Kiswahili Book for Peace Corps Tanzania.
INSTITUTION Peace Corps, Arusha (Tanzania).
PUB DATE Jun 94
NOTE 279p.
PUB TYPE Guides - Classroom Use - Instructional Materials (For Learner) (051)
LANGUAGE Swahili; English


EDRS PRICE MF01/PC12 Plus Postage.
DESCRIPTORS Conversational Language Courses; *Daily Living Skills; Foreign Countries; Grammar; *Interpersonal Communication; Second Language Instruction; *Second Language Learning; *Swahili; Uncommonly Taught Languages; Vocabulary Development; Voluntary Agencies; *Volunteer Training
IDENTIFIERS Peace Corps; Tanzania

ABSTRACT

This guide is designed for the Swahili language training of Peace Corps volunteers and focuses on daily communication needs in that context. It consists of a series of 76 lessons, each containing vocabulary and phrase lists, dialogue, grammar notes, and exercises. Lesson topics include: greetings and introductions; numbers; commands; questions; expressing time; family; shopping; daily activities; getting and giving directions; the human body; health; housing; banking; weather; agriculture; colors; festivals; transportation; and travel. A Swahili-to-English glossary and list of useful phrases are appended. (MSE)

* Reproductions supplied by EDRS are the best that can be made *
* from the original document. *

ED 402 737



U.S. DEPARTMENT OF EDUCATION
Office of Educational Resources and Improvement
EDUCATIONAL RESOURCES INFORMATION
CENTER (ERIC)

- This document has been reproduced as received from the person or organization originating it.
- Minor changes have been made to improve reproduction quality.
- Points of view or opinions stated in this document do not necessarily represent official OERI position or policy.

004285

BEST COPY AVAILABLE

KISWAHILI BOOK



FOR PEACE CORPS TANZANIA
JUNE 1994 - ARUSHA, TANZANIA

Written by

Esther M. Simba
Claudius N. Marshal
Hamisi K. M. Msumi
Kiobya Yahaya
Bazila A. Nyambo
Mohamed Kondo
Oswald M. Ngadatta
Jumapili M. Nyaruga

Secretarial work by
Mrs. Doreen P. Lyimo

Art Work by

Fred Kigallu
Charles Lwamlema
Lawrence Hinju
Benjamin Lulabuka
Theodore J. Domet



A C K N O W L E D G E M E N T

The authors of this book under the supervision of **Esther M. Simba** would like to give their sincere gratitude to the Peace Corps Country Director - **David Ashby**, Administrative Officer - **Mike Athens**, for their willingness in supporting and financing this book to be written. We also thank the former Associate Peace Corps Director for Education - **Sharon Johns** for her patience, flexibility and advice which contributed to the success of this book. The Peace Corps staff in Dar and Arusha training site would not be forgotten for their inputs in one way or another. Last but not least, the Training Director **Joan Bordman** can not be left behind for her encouragement in writing this book. It is not easy to thank everybody individually but we would like them to accept our heartfelt gratitude. Since this is a pilot book, we would like to invite any additional contributions to improve it.

P R E F A C E

Communication is one of the most important thing in any society. For that matter we (the authors) thought that there is a need of trying to write this book in order to ease communication between foreigners and Tanzanians especially those who work here in different fields. Since the common language in East Africa is Kiswahili, we have written this book sighting areas like conversation and structure (grammar) in a simpler way. The communication topics have been designed in such a way that vocabulary comes first followed by English translation, then Kiswahili conversation and lastly exercises. Grammar begins with the grammatical explanation, examples, exercises and vocabulary. The structure topics have been designed by giving explanation about the topic, followed by exercises and then vocabulary.

The aim of this book is to help Peace Corps volunteers who are working in Tanzania to bridge the communication gap, and also other Peace Corps staff who might be interested to learn this language. It is our expectation that by following the instructions put in this book and by doing the exercises you will learn this language in the easiest way.

We would like once again to thank all those who participated in the work of writing this book. And to the reader we invite more comments which will lead us to the last work of this book so that it can serve as many people as possible.

The Authors "



Table of Contents



	Page
1. Acknowledgement	i
2. Preface	ii
3. Greetings	1
4. Self Introduction	5
5. Numbers 0-1000	9
6. Personal Pronouns, Possessive Pronouns & Subject Prefixes (Singular)	11
7. What are you Doing in Tanzania?	15
8. Verb "to be" Present Positive and Negative	19
9. Commands	21
10. Present, Past and Future Tenses Singular	27
11. Question Words	31
12. Personal Pronouns, Possessive Pronouns & Subject Prefixes (Plural)	37
13. Useful Constructions	41
14. Days of the Week	43
15. Family Structure	45
16. Verb to have Present	49
17. Numbers 1001-100,000	51
18. Months and Dates	53
19. At the Market	59
20. Measurements	63
21. Verb "to have" Past and Future	65
22. Negative Present Singular and Plural	69
23. Negative Past Singular and Plural	73
24. Negative Future Singular and Plural	75
25. Negatives of the verb "to have"	77
26. My Friend	83

27. The "Me" Tense	87
28. Telling Time	91
29. Daily Activities	95
30. Giving and Receiving Directives	101
31. At the Shop	105
32. Verb to be Past and Future	109
33. Negative of the Verb "to be" Past and Future	113
34. M-/Wa- Noun Class	115
35. Ji-/Ma- Noun Class	119
36. Parts of the Body	121
37. At the Hospital	125
38. Object Infixes	129
39. Passives	133
40. At my Home	137
41. Subjunctives	141
42. '-Po-' as When	143
43. Past Events	145
44. At the Hotel	149
45. Locative Suffixes -Ko -Po -Mo	153
46. Ki-/Vi- Noun Class (ch-/vy-)	157
47. Place Words	159
48. M-/Mi- Noun Class	163
49. At the Post Office	165
50. "Amba-" Relative Clauses	171
51. N-/N- Noun Class	177
52. The Uses of "Kwa"	181
53. At the Bank	183
54. U-/N- Noun Class	187
55. Mahali Class	191
56. Reciprocal Verbs	193
57. Adjectives with "Consonant Stems"	197
58. Compass Direction	201
59. Weather and Agriculture in Tanzania	203
60. -Engi and -Ingi	207
61. -Engine and -Ingene	209
62. Wild Animals of Tanzania	213

63. Adjectives with "Vowel Stem"	217
64. "Ki"/"Kama" as "If"	219
65. The Negative of "-Ki-" as "If" ("Sipo")	223
66. "-Nge-"/"-Ngali-"	225
67. Tanzanian	227
68. Colours	231
69. Festivals	235
70. "-Isha-" and "-Ja-" Using "-Me-" Tense	239
71. Noun Class Agreement Chart	241
72. Reflexive Infix "-Ji-" as Self/Selves	243
73. At a Tanzanian's Home	245
74. "-Vyo-" as "How"	249
75. Transport in Tanzania	251
76. Brian's Journey	255
77. Adjectives of Arabic Origin	259
78. Glossary	261
79. Kiswahili Useful Phrases	274

GREETINGS

Msamiati:	- vocabulary
<i>habari</i>	- news
<i>nzuri</i>	- fine, good
<i>salama</i>	- fine, good, peacefully
<i>hodi ! hodi!</i>	- may I come in?
<i>njema</i>	- fine, good
<i>shikamoo</i>	- how are you elder, I respect you elder
<i>marahaba!</i>	- fine, good, I accept
<i>mzima?</i>	- are you fine?
<i>mambo?</i>	- how are things?
<i>u-hali gani?</i>	- how are you?
<i>umeshindaje?</i>	- how has the day been?
<i>umelalaje?</i>	- how have you slept?
<i>umeamkaje?</i>	- how have you waken up?




Tatu:	May I come in?
Baraka:	You are welcome.
Tatu:	Thanks.
Baraka:	Have a seat.
Tatu:	Thank you.
Baraka:	How are you?
Tatu:	I am fine.
Baraka:	How is home?
Tatu:	Fine, how is it here?
Baraka:	Good/ <i>Fine</i>

Other Greetings

- | | |
|---------------------------------|-------------------|
| 1. Are you fine? | - Fine. |
| 2. I respect you elder? | - I accept. |
| 3. Are you fine? | - Fine |
| 4. How are things? | - Fine |
| 5. How did you conquer the day? | - Fine |
| 6. How have you slept? | - Fine |
| 7. How have you waken up? | - Fine |
| 8. (Name) what's up? | - Fine |
| 9. How are things? | - Things are fine |

N.B: Historically Shikamoo, meant may I hold your feet? And Marahaba meant Yes you may.

SALAMU



Tatu:	Hodi! Hodi!
Baraka:	Karibu.
Tatu:	Asante.
Baraka:	Karibu kiti
Tatu:	Asante.
Baraka:	Hujambo?
Tatu:	Sijambo.
Baraka:	Habari za nyumbani?
Tatu:	Nzuri, habari za hapa?
Baraka:	Nzuri.



Salamu nyingine

Salamu	Jibu	Hali (Situations)
Greetings	Responses	
1. Salama?	Salama.	- friends
2. Shikamoo!	Marahaba!	- said in response to an older person
3. Mzima?	Mzima.	- people you know in the same class
4. Mambo?	Safi/doi.	- friends
5. Umeshindaje?	Salama.	- people of the same age - afternoon
6. Umelalaje?	Salama.	- second greeting
7. Umeamkaje?	Salama.	- second greeting
8. (Jina) Vipi?	Safi.	- friends
9. Mambo vipi?	Mambo si.	- friends

Mazoezi

A. Tafuta majibu sahihi kwa salamu zifuatazo: (Find the appropriate responses for the following greetings)

1. Habari gani? _____
2. Hujambo? _____
3. Salama? _____
4. Mzima? _____
5. Shikamoo! _____

B. Tafuta salamu kwa majibu yafuatayo: (Find the greetings for the following responses)

1. _____? Mzima.
2. _____? Salama kabisa.
3. _____? Nzuri.
4. _____? Njema tu.
5. _____? Safi.
6. _____? Sijambo.
7. _____? Marahaba.
8. _____? Nzuri.
9. _____? Asante

C. Maliza sentensi zifuatazo: (Complete the following sentences)

1. Jina langu ni _____.
2. Ninatoka _____.
3. Ninatoka jimbo la _____.
4. Mimi ni _____.
5. Sasa ninakaa _____.

D. Andika mazungumo ya watu wawili: (Write a dialogue of two people)

Brian: _____.

Suzan: _____.

SELF INTRODUCTION

Msamiati:

<i>irwa</i>	-	<i>be called</i>
<i>mgeni</i>	-	<i>a visitor, guest, foreigner, stranger</i>
<i>jimbo</i>	-	<i>state or province</i>
<i>baba</i>	-	<i>father</i>
<i>mama</i>	-	<i>mother</i>
<i>toka</i>	-	<i>be from</i>
<i>mkoa</i>	-	<i>region</i>
<i>kaa</i>	-	<i>stay, live</i>
<i>nani?</i>	-	<i>who, what, whom?</i>
<i>wapi?</i>	-	<i>where?</i>
<i>gani?</i>	-	<i>which, what kind of, what type?, what sort of?</i>
<i>kaka</i>	-	<i>brother</i>
<i>dada</i>	-	<i>sister</i>

Tatu:	How are you today?
Brian:	Fine.
Tatu:	What is your name?
Brian:	My name is Brian.
Tatu:	Where are you from?
Brian:	I am from America.
Tatu:	Which state are you from?
Brian:	I am from Minesota.
Tatu:	Are you a visitor in Tanzania?
Brian:	Yes. I am a visitor in Tanzania.
Tatu:	Welcome to Tanzania.
Brian:	Thank you.

KUJITAMBULISHA



Tatu: Habari za leo?
Brian: Nzuri.
Tatu: Unaitwa nani?
Brian: **Ninaitwa Brian.**
Tatu: Unatoka wapi?
Brian: **Ninatoka Marekani.**
Tatu: Unatoka jimbo gani?
Brian: **Ninatoka jimbo la Minesota.**
Tatu: Wewe ni mgeni Tanzania?
Brian: **Ndiyo, mimi ni mgeni Tanzania.**
Tatu: Karibu Tanzania.
Brian: Asante.

Mazoezi

A. Jibu maswali haya: (Answer these questions)



1. Wewe unaitwa nani?

2. Yeye anaitwa nani?

3. Baba yako anaitwa nani?

4. Mama yako anaitwa nani?

5. Dada yako anaitwa nani?

6. Brian anatoka wapi?

7. Brian anatoka jimbo gani?

8. Brian ni nani?

9. Wewe unatoka jimbo gani?

10. Kaka yako anaitwa nani?



*Jina langu ni Baraka.
Ninatoka Tanzania.
Ninatoka mkoa wa Mwanza.
Mimi ni Msukuma.
Sasa ninakaa Dar es Salaam.*



B. Jibu maswali kutokana na picha ya hapo juu: (Answer questions using the picture above)

1. Jina lake ni nani?

2. Anatoka wapi?

3. Anatoka mkoa gani?

4. Yeye ni nani?

5. Sasa anakaa wapi?

6. Wewe unakaa wapi?

7. Je Baraka anatoka Tanzania?

NUMBERS 0-1000

0 = sifuri	10 = kumi	100 = mia moja
1 = moja	20 = ishirini	200 = mia mbili
2 = mbili	30 = thelathini	900 = mia tisa
3 = tatu	40 = arobaini	1000 = elfu moja
4 = nne	50 = hamsini	
5 = tano	60 = sitini	
6 = sita	70 = sabini	
7 = saba	80 = themanini	
8 = nane	90 = tisini	
9 = tisa		

When the units are added to the tenth we get 'kumi na moja', 'kumi na mbili', ishirini na tatu, thelathini na moja wich literally means:- ten and one, ten and two, twenty and three, thirty and one etc.,

Mazoezi

A. Andika maneno haya katika tarakimu: (Write these words into numerals):

1. Tisini na tano

2. Themanini na sita

3. Elfu moja na moja

4. Hamsini na nne

5. Elfu moja na tano

6. Mia nane sabini na tano

7. Sabini na tisa

B. Andika namba zifuatazo kwa maneno: (Write the following numbers in words)

1. 999

2. 1009

3. 44

4. 35

5. 375

6. 444

7. 111

8. 88

9. 125

10. 804

C. Jaza nafasi zifuatazo kwa maneno: (Fill the following blanks in words)



20			50	
	65		85	
	200			500
		15		25

PERSONAL PRONOUNS, POSSESSIVE PRONOUNS & SUBJECT PREFIXES (SINGULAR)

In Kiswahili personal pronouns, possessive pronouns and subject prefixes singular are expressed as follows:

A. PERSONAL PRONOUNS (SINGULAR)

Mimi - I
Wewe - You
Yeye - He/She



B. POSSESSIVE PRONOUNS

- angu - my, mine
- ako - your, yours
- ake - his, her, its



C. SUBJECT PREFIXES (SINGULAR)

Mimi - Ni
Wewe - U
Yeye - A

Mfano:

Mimi ninatoka Marekani.

(I am from the US)

Wewe unatoka Tanzania.

(You are from Tanzania)

Yeye anatoka Uingereza.

(He/she is from UK)

M zoezi

A. Malizia majibu ya maswali yafuatayo: (Complete the answers for the following questions)

Brian: Unatoka wapi?

Tatu: Ninatoka _____

Brian: Unatoka mkoa gani?

Tatu: Ninatoka mkoa wa _____

Baraka: Anatoka wapi?

Tatu: Anatoka _____

Baraka: Anatoka jimbo gani?

Tatu: Anatoka jimbo la _____

B. Tunga sentensi kwa kutumia picha zifuatazo: (Make sentences by using the following pictures)

Mfano:



Mimi ninakula chakula.
Wewe unakula chakula.
Yeye anakula chakula.

1.



2.



3.



4.



5.



6.



WHAT ARE YOU DOING IN TANZANIA?

Msamiati:

<i>kazi</i>	-	<i>job, work</i>
<i>fanya</i>	-	<i>do</i>
<i>jifunza</i>	-	<i>learn, study</i>
<i>fundisha</i>	-	<i>teach</i>
<i>mwalimu</i>	-	<i>teacher</i>
<i>kwa heri</i>	-	<i>good-bye</i>
<i>ishi</i>	-	<i>live, stay</i>
<i>nchi</i>	-	<i>country</i>
<i>fikiri</i>	-	<i>think</i>
<i>nini?</i>	-	<i>what?</i>
<i>kemia</i>	-	<i>chemistry</i>
<i>fizikia</i>	-	<i>physics</i>
<i>hisabati</i>	-	<i>mathematics</i>
<i>baolojia</i>	-	<i>biology</i>



Baraka: How are you today?
Tatu: Fine. How is your work?
Baraka: Fine, which country do you come from?
Tatu: I come from _____.
Baraka: Where are you staying?
Tatu: I am staying at _____.
Baraka: What are you doing in Tanzania?
Tatu: I am now learning Kiswahili but later
I will teach _____.
Baraka: Oh! are you a teacher?
Tatu: Yes, I am a teacher.
Baraka: You are warmly welcome to Tanzania.
Tatu: Thank you very much.
Baraka: Good-bye!
Tatu: Good-bye!

UNAFANYA NINI TANZANIA?



Baraka: Habari za leo?

Tatu: Nzuri. Habari za kazi?

Baraka: Nzuri tu. Unatoka nchi gani?

Tatu: Ninatoka _____

Baraka: Unakaa wapi?

Tatu: Ninakaa _____

Baraka: Unafanya nini Tanzania?

Tatu: Sasa ninajifunza Kiswahili lakini baadaye nitafundisha _____

Baraka: Aha! wewe ni Mwalimu?

Tatu: Ndiyo mimi ni Mwalimu.

Baraka: Karibu sana Tanzania.

Tatu: Asante sana.

Baraka: Kwa heri.

Tatu: Kwa heri.

Mazoezi

A. Tumia jedwali hili kuunda sentensi: (Use this chart to construct sentences)

Jina		Nchi	Jimbo	Anakaa	Kazi
Brian		Marekani	New York	Arusha	Mwalimu wa baolojia
Baraka	Mimi	Tanzania	Dodoma	Mwanza	Mwalimu wa fizikia
Suzana	Wewe	Marekani	California	Iringa	Mwalimu wa kemia
John	Yeye	Tanzania	Morogoro	Dar es Salaam	Mwalimu wa hisabati

Mfano:

Mimi ni Brian, ninatoka Marekani jimbo la New York. Sasa ninakaa Arusha. Mimi ni mwalimu wa Baolojia. Ninafanya kazi Peace Corps.

Mimi _____

Wewe _____

Yeye _____

B. Jibu maswali yafuatayo: (Answer the following questions)

1. Baraka alizungumza na nani?

2. Unafikiri Baraka anatoka wapi?

3. Sasa Tatu anafanya nini Tanzania?

4. Baadaye Tatu atafanya nini Tanzania?

5. Baadaye wewe utafanya nini Tanzania?



**C. Andika mazungumzo kuhusu unafanya nini Tanzania:
(Write a dialogue about what you are doing in Tanzania)**

VERB "TO BE" PRESENT POSITIVE AND NEGATIVE

The verb "to be" in Kiswahili is irregular which means it changes according to the tenses referred to. In the present tense the verb "to be" is denoted by "ni" for all personal pronouns and its negative is denoted by "si".

Mfano: Mimi ni Mmarekani.	- (I am an American.)
Wewe ni Mtanzania.	- (You are a Tanzanian.)
Yeye ni Mwingereza.	- (S/he is British.)
Mimi ni Brian.	- (I am Brian.)
Wewe ni Tatu.	- (You are Tatu.)
Yeye ni Baraka.	- (He is Baraka.)
Yeye ni Brian?	- (Is he Brian?)
Hapana. Yeye si Brian.	- (No. He is not Brian.)
Wewe ni Tatu?	- (Are you Tatu?)
Ndiyo. Mimi ni Tatu.	- (Yes. I am Tatu.)
Mimi ni Baraka?	- (Am I Baraka?)
Hapana. Wewe si Baraka.	- (No. You are not Baraka.)
Wewe ni Brian?	- (Are you Brian?)
Ndiyo. Mimi ni Brian.	- (Yes. I am Brian.)

Mazoezi

A. Kwa kutumia mfano ufuatao jibu maswali haya: (Using the example given answer the following questions)

Mfano: A. Yeye **ni** Mwalimu?
B. **Ndiyo.** Yeye **ni** mwalimu.

1. A. Wewe ni mtoto?
B. _____
2. A. Mimi ni mwanafunzi?
B. _____
3. A. Wewe ni Mtanzania?
B. _____



David




Baraka



Cheng



Ole Saitabau



Tatu

B. Kwa kutumia 'ni' na 'si' andika sentensi nane kutokana na picha za hapo juu: (Using the verb 'to be' in present and its negative construct eight sentences using the above pictures)

1. David ni Mwalimu?

2. Cheng ni Mchina?

3. Tatu ni Daktari?

4. Ole Saitabau ni Mmasai?

5. David ni Daktari?

6. Cheng ni mwanafunzi?

7. Baraka ni Mchina?

Msamiati:

- daktari - doctor
- mmasai - a masai
- mwanafunzi - student
- mchina - a chinese

COMMANDS

When verb roots are used alone without any subject or object concords they are called **commands**. Normally these commands are used when one orders a person to do something.

Mfano:	kula	-	eat
	lala	-	sleep
	kunywa	-	drink
	amka	-	wake up, get up
	soma	-	read
	angalia	-	look, watch
	fikiri	-	think
	andika	-	write
	sikiliza	-	listen
	piga mswaki	-	brush teeth
	oga	-	bathe
	vaa nguo	-	dress
	vua nguo	-	undress
	pika	-	cook
	zungumza	-	talk, converse
	washa taa	-	switch on the light, put on the light, light the lantern
	zima taa	-	switch off light, put off light, put off the lantern
	fagia	-	sweep
	safisha	-	clean
	fua	-	wash



Mazoezi

A. Fasiri maneno yafuatayo: (Translate the following words)

Mfano:	read	soma
1.	eat	_____
2.	think	_____
3.	sleep	_____
4.	write	_____
5.	look	_____

- 6. listen _____
- 7. wake up _____
- 8. drink _____

B. Jaza nafasi zilizo wazi kwa kutumia vitenzi sahihi: (Fill in the blanks by using appropriate verbs)

- 1. Jana mimi nili _____ ndizi.
- 2. Mtoto ana _____ radio.
- 3. Brian ata _____ soda baridi.
- 4. Tatu ali _____ gazeti.
- 5. Baraka ana _____ video.
- 6. Suzana ali _____ barua.
- 7. Mwalimu ana _____ taa.
- 8. Kesho Baraka ata _____ mswaki.
- 9. Sasa Suzan ana _____ pizza.
- 10. Jana Brian ali _____ Kiswahili.

C. Tumia picha kujibu au kuuliza maswali: (Use the pictures to answer or to ask questions)

Mfano:



Swali: Ulifanya nini?
Jibu: Nilisoma

1.



Swali: _____ ?

Jibu: Nitaandika

2.



Swali: Nitafanya nini?

Jibu: _____

3.



Swali: Alifanya nini?

Jibu: _____

4.



Swali: Nilifanya nini?

Jibu: _____

5.



Swali: _____?

Jibu: Nitaoga.

6.



Swali: _____?

Jibu: Analala.

7.



Swali: Unafanya nini?

Jibu: _____

D. Jibu maswali haya: (Answer these questions)

1. Kabla ya kuja Tanzania ulifanya nini?

2. Utafanya kazi wapi?

3. Sasa wewe unafanya nini?

4. Jana baada ya kujifunza Kiswahili ulifanya nini?

5. Mwaka kesho utafanya nini?

6. Jumapili utafanya nini?

7. Kesho usiku utafanya nini?

8. Mwalimu anafanya nini?

9. Jana usiku baba alifanya nini?

10. Jumamosi usiku wewe utafanya nini?

11. Sasa mama yako anafanya nini?

12. Leo mchana utafanya nini?

13. Kesho jioni utafanya nini?

14. Jana usiku wewe ulifanya nini nyumbani?

15. Sasa rafiki yako anafanya nini?

Msamiati:

<i>chota maji</i>	-	<i>draw water</i>
<i>kata mti</i>	-	<i>cut tree</i>
<i>baada ya</i>	-	<i>after</i>
<i>kabla ya</i>	-	<i>before</i>
<i>jumapili</i>	-	<i>sunday</i>
<i>mchana</i>	-	<i>afternoon</i>
<i>jioni</i>	-	<i>evening</i>
<i>usiku</i>	-	<i>night</i>
<i>barua</i>	-	<i>letter</i>
<i>taa</i>	-	<i>lantern, lamp, light</i>
<i>radio</i>	-	<i>radio</i>
<i>ndizi</i>	-	<i>banana</i>
<i>baridi</i>	-	<i>cold</i>
<i>gazeti</i>	-	<i>news paper, magazine</i>
<i>mtoto</i>	-	<i>child, baby</i>

PRESENT, PAST AND FUTURE TENSES SINGULAR

There are four primary tenses in Kiswahili. *-na-*, *-ta-*, *-li-* & *-me-*.
But at this stage we will only deal with '*-na-*', '*-ta-*', and '*-li-*'.

-na- This tense refers to an action taking place now and an action which is continuing.

- Mfano:**
1. Sasa **Ninakunywa** chai
(Now I am drinking tea.)
 2. **Ninaandika** barua.
(I am writing a letter.)
 3. **Ninaangalia** mdudu.
(I am looking at an insect.)

-ta- A tense sign marker which stands for future tense.

- Mfano:**
1. Kesho **Nitakunywa** chai.
(Tomorrow I will drink tea.)
 2. **Nitaandika** kitabu.
(I will write a book.)
 3. **Nitasoma** barua.
(I will read a letter.)


-li- A tense sign marker which stands for simple past tense.

- Mfano:**
1. Jana **nilikunywa** chai.
(Yesterday I drank tea.)
 2. **Niliandika** barua
(I wrote a letter.)
 3. **Nilisoma** kitabu
(I read a book.)

Mazoezi

A. Jaza nafasi zifuatazo kwa kutumia nyakati sahihi: (Fill the following blanks by using appropriate tenses)

1. Mimi _____ kaa wapi? (jana)
2. Yeye _____ toka Marekani. (sasa)
3. Wewe _____ andika barua. (kesho)
4. Mimi _____ kunywa chai. (sasa)
5. Suzana _____ jifunza Kiswahili. (sasa)
6. Mama _____ kula chakula. (jana)
7. Mwalimu _____ fundisha Kiswahili. (kesho)
8. Mimi _____ nunua matunda. (sasa)
9. Wewe _____ utasikiliza redio. (kesho)
10. Mimi _____ soma gazeti. (jana)



B. Fasiri sentensi zifuatazo katika Kiswahili: (Translate the following sentences into Kiswahili)

1. You are watching video.

2. He was learning Kiswahili in the US.

3. I am going to town.

4. He is called Baraka.

5. I am reading a newspaper.

6. The student learned Kiswahili in Arusha.

7. Peter is talking to his teacher.

8. You listened to the music.

C. Tumia jedwali hili kutunga sentensi kumi: (Use this chart to construct ten sentences)

Jina	Jana	Sasa	Kesho
Baraka	kula chakula	soma gazeti	andika barua
Brian	cheza dansi	angalia video	piga pasi
Suzana	amka	zungumza	piga simu
Tabu	cheza mpira wa mikono	enda sokoni	nunua redio

Mfano: Baraka alikula chakula. - Baraka ate food.
Brian anaangalia video. - Brian is watching video.
Suzana atapiga simu. - Suzana will make a phone call.

1. _____
2. _____
3. _____
4. _____
5. _____
6. _____
7. _____
8. _____
9. _____
10. _____

D. Fasiri sentensi zifuatazo katika Kiswahili: (Translate the following sentences into Kiswahili)

1. I listened to the radio.

2. You are watching video.

3. Tatu will eat bananas.

4. Baraka is learning Kiswahili.

5. Brian brushed teeth.

Msamiati:

- | | | |
|-----------------------|---|----------------------|
| <i>sokoni</i> | - | <i>at the market</i> |
| <i>soko</i> | - | <i>market</i> |
| <i>cheza</i> | - | <i>play</i> |
| <i>mpira</i> | - | <i>ball</i> |
| <i>mpira wa mkono</i> | - | <i>hand ball</i> |
| <i>nunua</i> | - | <i>buy</i> |
| <i>piga pasi</i> | - | <i>ironing</i> |
| <i>pasi</i> | - | <i>an iron</i> |

QUESTION WORDS

In Kiswahili language there are different question words which are used to ask questions. When asking a question the intonation changes by raising up the voice. These question words are as follows:

- | | | | |
|-----------------|---|---------------------------------------|---|
| 1. Nani? | - | What, who, whom? | |
| 2. Wapi? | - | Where? | |
| 3. Kwa nini? | - | Why?, for what? | |
| 4. Lini? | - | When? | |
| 5. Mbona? | - | Why?, how come? | |
| 6. Ngapi? | - | How many?, how much? | |
| 7. Gani? | - | What sort of?, which?, which kind of? | - |
| 8. Nini? | - | What? (used for objects only) | - |
| 9. Vipi? | - | How? | |
| 10. Namna gani? | - | How?, how is it? | |

The Particle "je"

When "Je" is used at the beginning of the sentence it draws attention i.e. the question is coming.

Mfano:

Je, utakwenda mjini leo? - Will you go to town today?

*When "je" is used at the end of the verb it means **how**.*

Mfano:

Wewe utakwendaje mjini? - How will you go to town?

When "je" is used at the end of the noun it means what about/how about, but it should be preceded by a phrase giving prior information.

Mfano: Mimi ninatoka Tanzania - I am from Tanzania
wewe je? what about you?
Sisi tutakwenda sokoni - We will go to the market
kesho, wao je? tomorrow what about them?

Mifano zaidi:

- | | | |
|-----------------------------------|---|---------------------------------|
| 1. Kwa nini unajifunza Kiswahili? | - | Why are you learning Kiswahili? |
| 2. Jina lako ni nani? | - | What is your name? |

- | | | |
|----------------------------------|---|---------------------------------|
| 3. Kila siku unajifunza nini? | - | What are you learning everyday? |
| 4. Utakwendaje mjini? | - | How will you go to town? |
| 5. Je, utajifunza Kiswahili leo? | - | Will you learn Kiswahili today? |

Mazoezi

- A. Soma habari ifuatayo halafu jibu maswali hapo chini:(Read the following passage and answer the questions below)**

Juzi jioni nilikwenda sokoni. Nilikwenda sokoni pamoja na rafiki yangu Brian. Tulikwenda kwa pikipiki. Tulikwenda sokoni kununua matunda. Brian alinunua ndizi 10 lakini mimi nilinunua ndizi 20. Bei ya ndizi moja ni shilingi 5/=.

Maswali.

1. Juzi nilikwenda wapi?

2. Nilikwenda pamoja na nani?
-

3. Je juzi nilikwenda sokoni?
-

4. Mimi na Brian tulikwendaje sokoni?
-

5. Mimi nilinunua ndizi ngapi?
-

6. Brian je?
-

7. Sokoni tulinunua nini?
-

8. Tulinunua matunda gani sokoni?
-

9. Kwanini mimi na Brian tulikwenda sokoni?

10. Tulikwenda sokoni lini?

B. Soma habari ifuatayo halafu tunga maswali kumi na tano: (Read the following passage then construct fifteen questions)

Baraka na Suzana ni marafiki sana. Baraka anakaa Dar es Salaam na Suzana anaishi Arusha. Siku ya Jumamosi Suzana alikwenda Dar es Salaam kumtembelea Baraka. Baraka alifurahi sana kumwona Suzana na Suzana pia alifurahi sana. Siku ya Jumatatu Suzana alirudi Arusha kwa basi la 'Royal Sumayi.'

Mfano:

Rafiki yake Baraka jina lake ni nani?

1. _____ ?
2. _____ ?
3. _____ ?
4. _____ ?
5. _____ ?
6. _____ ?
7. _____ ?
8. _____ ?
9. _____ ?
10. _____ ?
11. _____ ?
12. _____ ?
13. _____ ?

14. _____ ?

15. _____ ?

C. Jibu maswali 10 ya zoezi B: (Answer 10 questions from exercise B)

Mfano:

Rafiki yake Baraka jina lake ni Suzana.

1. _____

2. _____

3. _____

4. _____

5. _____

6. _____

7. _____

8. _____

9. _____

10. _____

D. Jibu maswali yafuatayo: (Answer the following questions)

1. Unatoka wapi?

2. Kaka yako jina lake ni nani?

3. Kabla ya kuja Tanzania ulifanya nini?

4. Unapenda kula chakula gani?

5. Kwa nini unajifunza Kiswahili?

6. Unakulaje chakula?

7. Je, utakwenda mjini leo?

8. Sokoni Tanzania kuna matunda gani?

9. Kila siku unakwendaje nyumbani?

10. Je, unapenda kula ugali?

E. Andika maswali ya majibu yafuatayo: (Write questions for the following answers)

1. _____? Ninatoka mji wa Arusha.

2. _____? Tulikuja Tanzania kwa ndege.

3. _____? Wana shilingi mia tatu.

4. _____? Mnakunywa kahawa.

5. _____? Kwa sababu ninapenda kuzungumza Kiswahili na Watanzania.

6. _____? Atakwenda Dodoma kesho.

7. _____? Ndiyo mimi ni mtanzania.

8. _____? Yeye ni mwalimu.

Msamiati:



<i>kwenda</i>	-	<i>to go</i>
<i>sokoni</i>	-	<i>at the market</i>
<i>pamoja na</i>	-	<i>together with</i>
<i>pikipiki</i>	-	<i>motorcycle</i>
<i>kwa sababu</i>	-	<i>because</i>
<i>ruḍi</i>	-	<i>return</i>
<i>ishi</i>	-	<i>live</i>
<i>taka</i>	-	<i>want</i>
<i>kununua</i>	-	<i>to buy</i>
<i>rafiki</i>	-	<i>friend</i>
<i>matunda</i>	-	<i>fruits</i>
<i>ndizi</i>	-	<i>bananas</i>
<i>bei</i>	-	<i>price</i>
<i>tembelea</i>	-	<i>visit</i>

PERSONAL PRONOUNS, POSSESSIVE PRONOUNS AND SUBJECT PREFIXES (PLURAL)

In Kiswahili personal pronouns, possessive pronouns and subject prefixes plural are expressed as follows:

A. PERSONAL PRONOUNS

- Sisi - We, us
- Ninyi - You, (plural)
- Wao - They, them



B. POSSESSIVE PRONOUNS (PLURAL)

- etu - our, ours
- enu - your, yours
- ao - their, theirs



C. SUBJECT PREFIXES

- tu - we
- m - you (pl)
- wa - they, them

Mfano:

- Sisi tunatoka Marekani. - We are from US.
- Ninyi mnatoka Tanzania. - You are (pl) from Tanzania.
- Wao wanatoka Uingereza. - They are from UK.

Mazoezi

A. Malizia sentensi zifuatazo kwa kutumia 'subject prefixes' na 'tense sign maker': (Complete the following sentences using subject prefixes and 'tense sign marker')

1. Sisi _____ sema Kiswahili kila siku.
2. Ninyi _____ pumzika kesho.
3. Wao _____ soma vitabu sana.
4. Julius _____ andika barua kesho.
5. Baraka _____ fikiri sana jana.
6. Mtoto _____ cheza mpira.
7. Mama _____ pika ugali.
8. Mimi _____ kunywa chai sasa.
9. Brian na Suzana _____ toka Marekani.
10. Tatu _____ a. galia video jana.

B. Andika sentensi zifuatazo kwa usahihi kwa kutumia subject prefixes sahihi: (Write the following sentences correctly using the appropriate subject prefixes)

1. Mtoto wanakula sana.

2. Wao atakuja kesho mchana.

3. Sisi mlifikiri sana jana.

4. Wewe na John alikula ugali jana.

5. Wao anapika chakula.

6. Sisi mnacheza ngoma.

7. Ninyi walikula ugali nyumbani.

8. Mimi na Brian alicheza mpira.

9. Suzan na David mnaangalia video.

10. Mwalimu na mimi walikwenda sokoni.

C. Fasiri sentensi zifuatazo katika Kiswahili: (Translate the following sentence into Kiswahili)

1. They are sleeping now.

2. She is eating pizza.

3. I am writing a letter.

4. We will sweep tomorrow.

5. You (plural) spoke slowly.

6. They are washing clothes now.

7. Father and mother are watching video.

8. She is teaching Kiswahili.

9. They will cook ugali and pizza.

10. We went to the market yesterday.

Msamiati:

<i>ugali</i>	-	<i>stiff porridge</i>
<i>ngoma</i>	-	<i>drum, traditional dance</i>
<i>wanafunzi</i>	-	<i>students, pupils</i>
<i>polepole</i>	-	<i>slowly</i>
<i>fagia</i>	-	<i>sweep</i>
<i>fua nguo</i>	-	<i>wash clothes</i>

USEFUL CONSTRUCTIONS

In Kiswahili there are verbs which are commonly used in daily conversations. For that matter we have decided to call them useful constructions. The following are the group representative.

-enda	-	go
-weza	-	be able, can
-taka	-	want
-penda	-	love, like
-omba	-	beg, ask for something
-elewa	-	understand
-jua	-	know
-hitaji	-	need
-pata	-	get



Mfano:

Anakwenda sokoni.	-	S/he is going to the market.
Utaweza kuogelea?	-	Will you be able to swim?
Wanataka kunywa maji.	-	They want to drink water.
Mtappenda kujifunza Kiswahili?	-	Will you (pl) like to learn Kiswahili?

Mazoezi

A. Tunga sentensi tano kwa kutumia maneno haya: (Construct five sentences using these words)

omba, elewa, jua, hitaji, pata

1. _____
2. _____
3. _____
4. _____
5. _____

B. Fasiri sentensi zifuatazo kwa Kiswahili: (Translate the following sentences into Kiswahili):

1. We were able to speak Kiswahili.

2. They understood Kiswahili.

3. I needed tea with sugar.

4. She can cook rice.

5. He is going to town.

C. Tumia maneno yafuatayo kukamilisha sentensi zifuatazo: (Use the following words to complete the following sentences)

enda, weza, taka, jua, hitaji, omba, penda, elewa

1. Mwalimu ana _____ kunifundisha Kiswahili.
2. Nili _____ kupika chakula cha mchana.
3. Kila siku asubuhi nina _____ kunywa chai kabla ya kwenda shule.
4. Sasa nina _____ kuzungumza Kiswahili.
5. Kesho asubuhi nita _____ mjini kununua kalamu.
6. Sita _____ kuandika barua kwa kaka yangu.

Msamiati:

ogelea - swim
maji - water
sukari - sugar
mchele - uncooked rice

DAYS OF THE WEEK

In Kiswahili days of the week are named according to the Arabic system, which means the first day of the week is Saturday and the last day is Friday. Yet the arrangement of the days follows English system as shown below:-

Jumatatu	-	Monday
Jumanne	-	Tuesday
Jumatano	-	Wednesday
Alhamisi	-	Thursday
Ijumaa	-	Friday
Jumamosi	-	Saturday
Jumapili	-	Sunday



Mazoezi

A. Jibu maswali yafuatayo: (Answer the following questions)

1. Taja siku za wiki.

2. Leo ni siku gani ?

3. Jana ilikuwa siku gani?

4. Kesho itakuwa siku gani?

5. Juzi ilikuwa siku gani?

6. Kesho kutwa itakuwa siku gani?

7. Ulikuwa Tanzania siku gani?

8. Mnajifunza Kiswahili siku gani?

9. Unapumzika siku gani ?

B. Fasiri sentensi zifuatazo: (Translate the following sentences)

1. He came on Monday.

2. We shall go on Tuesday.

3. The doctor is coming on Sunday.

4. I'm staying until Thursday.

5. We will eat bread on Monday.

6. I'm leaving on Saturday.

7. We learn Kiswahili everyday.

8. Today is Thursday.

9. Tomorrow will be Friday.

10. What was the day before yesterday.

Msamiati:

<i>ilikuwa</i>	- it was	<i>kaa</i>	- stay, live, sit, crab
<i>itakuwa</i>	- it will be	<i>mpaka</i>	- until, border
<i>gani</i>	- which, what, what kind of	<i>kabla</i>	- before
<i>ondoka</i>	- leave, depart		


FAMILY STRUCTURE

Msamiati:

<i>babu</i>	-	<i>grandfather</i>
<i>bibi</i>	-	<i>grandmother</i>
<i>shangazi</i>	-	<i>father's sister</i>
<i>mjomba</i>	-	<i>mother's brother</i>
<i>baba mkubwa</i>	-	<i>father's elder brother</i>
<i>baba mdogo</i>	-	<i>father's younger brother</i>
<i>mama mkubwa</i>	-	<i>mother's elder sister</i>
<i>mama mdogo</i>	-	<i>mother's younger sister</i>
<i>mke</i>	-	<i>wife</i>
<i>mume</i>	-	<i>husband</i>
<i>mzazi</i>	-	<i>a parent</i>
<i>binamu</i>	-	<i>cousin</i>
<i>mpwa</i>	-	<i>nephew</i>

I am Baraka. My father is Masanja and my mother is Kashinde. My grandfather is Mabula and my grandmother is Kaniki. My uncle is Shija and my aunt is Shida. My elder father is Masalu and my younger father is Malulu. My elder mother is Kahangi and my younger mother is Ugumba. My brother is Mashili and my sister is Tabu.

MUUNDO WA FAMILIA



Mimi ni Baraka. Baba yangu ni Masanja na Mama yangu ni Kashinde. Babu yangu ni Mabula na Bibi yangu ni Kaniki. Mjomba wangu ni Shija na Shangazi yangu ni Shida. Baba yangu mkubwa ni Masalu na Baba yangu mdogo ni Malulu. Mama yangu mkubwa ni Kahangi na Mama yangu mdogo ni Ugumba. Kaka yangu ni Mashili na Dada yangu ni Tabu.

MONTHS AND DATES

Months

In Kiswahili the months in a year are named as follows:

Mwezi wa kwanza	first month	Januari
Mwezi wa pili	second month	Februari
Mwezi wa tatu	third month	Machi
Mwezi wa nne	fourth month	Aprili
Mwezi wa tano	Fifth month	Mei
Mwezi wa sita	sixth month	Juni
Mwezi wa saba	seventh month	Julai
Mwezi wa nane	eighth month	Agosti
Mwezi wa tisa	nineth month	Septemba
Mwezi wa kumi	tenth month	Oktoba
Mwezi wa kumi na moja	eleventh month	Novemba
Mwezi wa kumi na mbili	twelfth month	Desemba

Mazoezi

A. Jibu maswali haya: (Answer these questions)

1. Mwaka mmoja una siku ngapi?

2. Mwezi gani ni baridi sana Marekani?

3. Mwaka mmoja una miezi mingapi?

4. Mwezi gani una siku 28 au 29?

C. Hawa ni nani?: (Who are these?)

Mfano:

Bibi ni mama wa baba.

Kaniki ni bibi wa Baraka.

1. Babu ni _____.
2. Mjomba ni _____.
3. Shangazi ni _____.
4. Masalu ni _____.
5. Malulu ni _____.
6. Kahangi ni _____.
7. Ugumba ni _____.
8. Mashili ni _____.
9. Tabu ni _____.

D. Kwa kutumia muundo wa familia sema kweli au uongo:
(Using the family structure say true or false)

1. Baba wa baba anaitwa babu _____
2. Dada wa mama ni mjomba _____
3. Kaka wa baba ni shangazi _____
4. Mama wa baba na mama wa mama ni bibi _____
5. Mama mdogo ni kaka mdogo wa baba _____
6. Baba ni mume wa dada _____
7. Babu ni mke wa bibi _____
8. Babu ni mume wa bibi _____
9. Dada wa Baba ni shangazi _____
10. Mke wa Babu ni mama _____

Mazoezi

A. Malizia sentensi zifuatazo: (Complete the following sentences)

1. Leo ni tarehe _____
2. Kesho itakuwa tarehe _____
3. Nilizaliwa tarehe _____
4. Krismasi ni tarehe _____
5. Mwaka mpya ni tarehe _____
6. Nilikuja Tanzania tarehe _____
7. Nilianza kujifunza Kiswahili tarehe _____
8. Nitamaliza kujifunza Kiswahili tarehe _____

B. Andika tarehe hizi kwa maneno: (Write these dates in words)

Mfano:

3/5 /1994

Tarehe tatu mwezi wa tano mwaka elfu moja mia tisa tisini na nne.

1. 6/10/1993

2. 15/3/1998

3. 19/11/1975

6. _____
7. _____
8. _____
9. _____
10. _____

B. Kamilisha sentensi zifuatazo ili zilete maana ya "kuwa na": (Complete the following sentences so that they mean "to have")

Mfano:

Mimi nina _____ (oga/kitanda)

Mimi nina kitanda

1. Mwalimu ana _____ (kalamu/fundisha)
2. Watoto wana _____ (mpira/cheza)
3. Baraka ana _____ (kunywa/dada)
4. Wao wana _____ (machungwa/zungumza)
5. Sisi tuna _____ (nanasi/andika)
6. Wewe una _____ (kitabu cha Kiswahili/pika)

C. Badili sentensi zifuatazo kuwa katika Kiswahili: (Change the following sentences into Kiswahili)

1. I have four children.

2. We have three chairs.

3. They have one car.

4. You have three radios.

5. S/he has four exercise books.

6. You (pl) have nine students.

1. Lini niliandika kitabu?

2. Lini nitakwenda baharini kuogelea?

3. Lini nilikwenda Ufaransa?

4. Lini nilizaliwa?

5. Lini mlifanya karamu?

6. Lini nilinunua gari?

7. Lini nilipata mtoto?

8. Lini nilisafiri?

9. Lini nilinunua nguo?

10. Lini nilipika wali?

B. Fasiri namba zifuatazo kwa Kiswahili: (Translate the following numbers in Kiswahili)

1. Twelve thousand

2. One thousand and sixty eight

3. Nine thousand and five hundred

4. Seven thousand and two hundred

5. Two thousand one hundred and fifty two

6. Three thousand and one

7. One thousand and twenty one

8. Thirty thousand and twenty two

9. Nine thousand and one

C. Andika kwa tarakimu: (Write in numerals)

1. Efu kumi na tano

2. Efu mbili mia tisa tisini na tisa

3. Laki moja

4. Efu themanini na mbili

5. Efu hamsini na nane

6. Efu hamsini na tisa

7. Efu kumi na moja mia moja kumi na moja

8. Efu moja mia tisa tisini na nne

9. Efu mbili mia nane themanini na tisa

AT THE MARKET

Msamiati:

<i>soko</i>	- market	<i>lipa</i>	- pay
<i>sokoni</i>	- at the market	<i>chukua</i>	- take
<i>pikipiki</i>	- motor cycle	<i>mboga</i>	- vegetables
<i>matunda</i>	- fruits	<i>kununua</i>	- to buy
<i>bei gani?</i>	- how much?	<i>fungu</i>	- pile
<i>muuzaji</i>	- seller	<i>halafu</i>	- then
<i>jumla</i>	- total	<i>malimau</i>	- lemons
<i>nipe</i>	- give me		

The day before yesterday Baraka went to the market. He went by motorcycle. He went to the market to buy vegetables and fruits. At the market he talked with a seller:

Baraka: How are you today?

Seller: I am fine. You are welcome.

Baraka: Thank you. I want to buy vegetables and fruits.

Seller: You are welcome. What fruits do you want to buy?

Baraka: I want to buy pawpaws, pineapples, oranges
bananas and lemons.

Seller: One pawpaw is 100/=-, a pineapple is 200/=-, and an
orange is 50/=-. Each banana is 20/=- and one lemon is
10/=-.

Baraka: Ok!. Give me three pawpaws and four pineapples.

Seller: Ok!. You will pay the total of one thousand and one
hundred shillings.

Baraka: Take this money and give me the fruits.

Seller: Thanks, take your fruits and welcome again.

Baraka: Thank you very much.

5. Mwezi mmoja una siku ngapi?

6. Mwezi Januari ni mwezi gani?

7. Agosti ni mwezi gani?

8. Wewe unapenda mwezi gani? Kwa nini?

9. Ulifika Tanzania mwezi gani?

10. Krismasi ni mwezi gani?

Dates

In Swahili language dates are indicated by the ordinary numbers whereby one tells the date first, then the month and lastly the year. The word 'tarehe' comes before the numbers.

e.g. Tarehe nane mwezi wa saba mwaka 1994 - 8th July 1994

Mfano:

Tarehe moja	-	the first date of the month
Tarehe nne	-	the fourth date of the month
Tarehe sita	-	the sixth date of the month
Tarehe kumi	-	the tenth date of the month
Tarehe kumi na tisa	-	the nineteenth date of the month
Tarehe thelathini na moja	-	the thirty first date of the month

Mazoezi

A. Jibu maswali yafuatayo: (Answer the following questions)

1. Nani alikwenda sokoni?

2. Baraka alikwendaje sokoni?

3. Baraka alizungumza na nani sokoni?

4. Kwa nini Baraka alikwenda sokoni?

5. Papai moja ni bei gani?

6. Baraka alilipa jumla shilingi ngapi kununua matunda?

7. Baraka alitaka kununua matunda gani?

8. Wewe unapenda kula matunda gani?

B. Tafsiri maneno yafuatayo: (Translate the following words)

1. To buy _____
2. Fruits _____
3. Vegetables _____
4. Pineapples _____
5. Oranges _____
6. Bananas _____
7. Lemon _____
8. Cabbage _____
9. Green pepper _____
10. Pile _____
11. Take _____
12. Total _____

4. 8/2/1995

5. 1/8/1991

6. 30/7/1980

C. Jibu maswali kwa kutumia chati uliyopewa: (Answer the questions by using the chart given)

Siku	Tarehe	Mwezi	Mwaka	Fanya
Jumapili	10	12	1998	Nitaogelea
Alhamisi	19	1	1991	Nilinunua gari
Ijumaa	30	11	1987	Niliandika kitabu
Jumamosi	25	12	1993	Nilinunua nguo
Jumatatu	6	8	1987	Nilisafiri
Jumanne	17	10	1992	Nilipika wali
Jumatano	3	5	1988	Nilipata mtoto
Alhamisi	9	9	1963	Nilifanya karamu
Ijumaa	24	4	1960	Nilizaliwa
Jumanne	30	11	1954	Nilikwenda ulaya

MEASUREMENTS

There are different measurements depending on what some one wants to measure:

A. Local Measurements

- gunia - a sack, gunny bag
- debe - a tin of 18 - 20 litres
- kibaba - a local container used to measure solid things like beans, rice etc. at the market/shop
- fungu - a pile/heap

B. Urefu (Length)

- sentimeta - centimetre
- meta - metre (m)
- kilomita - kilometre



Mfano:

- sentimeta 100 = meta 1
- meta 1000 = kilometa 1

C. Uzito (Weight)

- gramu - gram (g)
- kilogramu - kilogram (kg)

Mfano:

- gramu 100 = dekagramu 1

D. Ujazo (Volume)

- lita - litre (l)

Mazoezi

A. Jibu maswali haya: (Answer these questions)

1. Sukari gramu 5000 ni kilo ngapi?

2. Debe moja ni lita ngapi?

3. Nusu kilo ni gramu ngapi?

4. Gramu 100 ni kilo ngapi?

5. Robo kilo ni gramu ngapi?

Msamiati:

<i>anza</i>	-	<i>start, begin</i>
<i>maliza</i>	-	<i>finish, complete</i>
<i>zaliwa</i>	-	<i>be born</i>
<i>mwaka mpya</i>	-	<i>new year</i>
<i>karamu</i>	-	<i>party</i>
<i>ogelea</i>	-	<i>swim</i>
<i>safiri</i>	-	<i>travel</i>
<i>bahari</i>	-	<i>sea, ocean</i>
<i>mwezi</i>	-	<i>month, moon</i>
<i>miezi</i>	-	<i>months, moons</i>
<i>mwaka</i>	-	<i>year</i>
<i>tarehe</i>	-	<i>date</i>
<i>Ufaransa</i>	-	<i>France</i>

VERB "TO HAVE" PAST AND FUTURE

The verb to have past and future in Kiswahili language is denoted by "kuwa na".

The verb "to have" Past

Mfano:

Nilikuwa na	-	I had
Ulikuwa na	-	You had
Alikuwa na	-	S/he had
Talikuwa na	-	We had
Mlikuwa na	-	You (pl) had
Walikuwa na	-	They had



Mifano zaidi:

Jana nilikuwa na nanasi
Juzi ulikuwa na kitabu
Mwaka jana Brian alikuwa na baiskeli

The verb "to have" Future

Mfano:

Nitakuwa na	-	I shall have
Utakuwa na	-	You will have
Atakuwa na	-	S/he will have
Tutakuwa na	-	We will have
Mtakuwa na	-	You (pl) will have
Watakuwa na	-	They will have

Mifano zaidi:

Kesho mimi nitakuwa na kitabu.
Kesho wewe utakuwa na kitabu.
Kesho yeye atakuwa na kitabu.
Kesho tutakuwa na kitabu.
Kesho Mtakuwa na kitabu.
Kesho watakuwa na kitabu.

SOKONI



Juzi Baraka alikwenda Sokoni. Alikwenda kwa pikipiki. Alikwenda sokoni kununua mboga na matunda. Sokoni alizungumza na muuzaji:

Baraka: Habari za leo?

Muuzaji: Nzuri, karibu!

Baraka: Asante sana. Ninataka kununua mboga na matunda.

Muuzaji: Karibu sana. Unataka kununua matunda gani?

Baraka: Ninataka kununua mapapai, mananasi, machungwa, ndizi na malimau.

Muuzaji: Papai moja ni shilingi 100/=, nanasi moja ni shilingi 200/= na chungwa moja ni shilingi 50/= . Kila ndizi ni shilingi 20/= na limau moja ni shilingi 10/=.

Baraka: Sawa, nipe mapapai matatu na mananasi manne.

Muuzaji: Sawa, jumla utalipa shilingi elfu moja na mia moja.

Baraka: Chukua pesa hizi na nipe matunda.

Muuzaji: Asante, chukua matunda yako na karibu tena.

Baraka: Asante sana.

B. Kamilisha sentensi zifuatazo ili zilete maana ya "kuwa na": (Complete the following sentences so that they mean "to have")

1. Nitakuwa na _____ (imba/keki)
2. Watakuwa na _____ (daftari/andika)
3. Mtakuwa na _____ (chungwa/kunywa)
4. Atakuwa na _____ (chakula/piga mswaki)
5. Wewe utakuwa na _____ (pikipiki/oga)


C. Tumia jedwali ulilopewa kutengeneza sentensi kumi:
(Using the chart given to construct ten sentences)


PERSONAL PRONOUNS	SUBJECT PREFIXES	PRESENT	PAST	FUTURE	NOUNS
Mimi	ni-				Nyumba
Wewe	u-				Kitabu
Yeye	a-				Mananasi
Sisi	tu-	-na-	-li-	-ta-	Machungwa
Nyinyi	m-		kuwa	kuwa na	Barua
Wao	wa-		na		Pikipiki
					Taa
					Gari
					Saa
					Ndege
					Kalamu
					Viti

C. Andika maneno haya kwa usahihi: (Write these words correctly)


1. TUAMDNA _____
2. UANNU _____
3. IPLIPLII _____
4. PMAPIAA _____
5. SINAMANA _____
6. WACHAMUNG _____
7. BOMGA _____
8. ZINDI _____
9. CHIBIKA _____
10. TIKAOR _____

D. Andika majina ya picha zifuatazo: (Write the name of the following pictures)














NEGATIVE PRESENT SINGULAR AND PLURAL

In negative present, no tense sign is used and if the last vowel is an "a" it is changed to an "i" and the negative subject prefixes are used.

Mfano: Affirmative	Negative
Sasa mimi ninaandika. (Now I am writing.)	- Sasa mimi siandiki. (Now I am not writing.)
Sasa wewe unaandika. (Now you are writing.)	- Sasa wewe huandiki. (Now you are not writing.)
Sasa yeye anaandika. (Now she/he is writing.)	- Sasa yeye haandiki. (Now she/he is not writing.)
Sasa sisi tunaandika. (Now we are writing.)	- Sasa sisi hatuandiki. (Now we are not writing.)
Sasa ninyi mnaandika. (Now you (pl) are writing.)	- Sasa ninyi hamwandiki. (Now you (pl) are not writing.)
Sasa wao wanaandika. (Now they are writing.)	- Sasa wao hawaandiki. (Now they are not writing.)

Note: 1

Whenever a consonant 'm' is preceded by verb stem vowels -w- is inserted between the consonant and the vowels.

Mfano: Affirmative	Negative
Sasa ninyi mnaandika	Sasa ninyi hamwandiki

Note: 2

Monosyllabic verbs like kula, kunywa, kuja, kwenda, drop the infinite 'ku' in negative present.

Mfano: Affirmative	Negative
Mimi ninakula samaki. (I am eating fish.)	- Mimi sili samaki. (I am not eating fish.)
Wewe unakunywa pombe. (You are drinking alcohol.)	- Wewe hunywi pombe. (You are not drinking alcohol.)
Sisi tunakwenda mjini. (We are going to town.)	- Sisi hauendi mjini. (We are not going to town.)

6. Tunaweza kupima nini kwa kutumia gunia?

B. **Tunga maswali na majibu kwa maneno yafuatayo:**
(Construct questions and answers to the following words)

Mfano:

Meta 10 ni sentimeta ngapi?

Meta 10 ni sentimeta 10,000.

1. Nusu kilo (a) _____
(b) _____
2. Nusu lita (a) _____
(b) _____
3. Sentimeta (a) _____
(b) _____
4. Kilo (a) _____
(b) _____
5. Gunia (a) _____
(b) _____
6. Gramu (a) _____
(b) _____
7. Debe (a) _____
(b) _____
8. Robo lita (a) _____
(b) _____
9. Fungu (a) _____
(b) _____
10. Lita (a) _____
(b) _____

Msamiati

- nusu* - half
robo - quarter
robo tatu - three quarters
kupima - to weigh, to measure, to diagnose, to examine
weza - be able to
kutumia - to use

C. Tumia jedwali ulilopewa hapo chini kutengeneza sentensi kumi katika kukataa: (Use the substitution table given below to construct ten sentences in the negative)

Sasa	mimi	si-	kunywa
	wewe	hu-	-zungumza
	yeye	ha-	-angalia
	sisi	hatu-	-lala
	nyingi	ham-	-sikiliza
	wao	hawa-	-pika

Mfano:

1. Sasa mimi sinywi bia (Now I am not drinking beer.)
2. Sasa mimi sipiki ugali (Now I am not cooking ugali)

1. _____
2. _____
3. _____
4. _____
5. _____
6. _____
7. _____
8. _____
9. _____
10. _____

A. Fasiri sentensi zifuatazo kwa Kiswahili: (Translate the following sentences into Kiswahili)

1. Tomorrow we will have one car.

2. The day before yesterday I had four pineapples.

3. The day after tomorrow I will have a bicycle.

4. Last year I had one house.

5. They will have a motor bike.

6. 1992 they had three bicycles.

7. You (pl) will have six pens.

8. You had three chairs.

9. She/He will have an exercise books.

10. I will have six pineapples.

NEGATIVE PAST SINGULAR AND PLURAL

The negative past is made by changing the past tense marker '-li-' into '-ku-' with the negative prefixes.

Mfano:

1. Jana asubuhi mimi sikupiga mswaki.
(Yesterday morning I didn't brush teeth.)
2. Wiki jana Brian hakuandika barua.
(Last week Brian didn't write a letter.)
3. Mwaka uliopita wanafunzi hawakuangalia video.
(Last year the students didn't watch video.)
4. Mwezi wa juzi sisi hatukulala nyumbani.
(Two months ago we didn't sleep at home.)



Mazoezi

A. Badili sentensi zifuatazo katika kukataa: (Change the following sentences into Negative)

1. Juzi Tatu alipika ugali.

2. Mwaka 1992 Brian na David walijifunza Kiswahili Arusha.

3. Jana ninyi mlikula samaki.

4. Wiki iliyopita sisi tulikunywa bia.

5. Juzi jioni mimi niliangalia sinema.

Mfano:

Mimi nina nyumba.

1. _____
2. _____
3. _____
4. _____
5. _____
6. _____
7. _____
8. _____
9. _____
10. _____

Msamiati:

<i>kitabu</i>	-	<i>a book</i>
<i>gari</i>	-	<i>a car, vehicle</i>
<i>baiskeli</i>	-	<i>a bicycle</i>
<i>kalamu</i>	-	<i>a pen</i>
<i>daftari</i>	-	<i>an exercise book</i>
<i>saa</i>	-	<i>watch, clock, time</i>
<i>viti</i>	-	<i>chairs</i>

NEGATIVE FUTURE SINGULAR AND PLURAL

The Negative Future is made by using the Future Tense with the Negative prefix:

Mfano:

Kesho mimi sitaenda ofisini
Tomorrow I won't go to the office

Mwaka kesho kutwa hawatacheza mpira.
Two years later they won't play soccer



Mazoezi

A. Badili sentensi hizi kwa kukataa: (Change these sentences in Negative)

1. Mwezi ujao Baraka na Tatu watacheza muziki.

2. Kesho usiku baba atakunywa pombe.

3. Wiki ijayo mimi nitafanya mtihani.

4. Mwaka kesho kutwa wewe utanunua gari.

